



TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT KWA LAZIMA (MUJIBU WA SHERIA) MWAKA 2024 AWAMU YA PILI

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, hivi karibuni alitoa wito kwa Vijana wahitimu wa elimu ya kidato cha sita mwaka 2024 kujiunga na mafunzo ya JKT kwa Lazima (Mujibu wa Sheria) kwa mwaka 2024.

Vijana hao walitakiwa kuripoti Makambi ya JKT waliyopangiwa kuanzia tarehe 01 Juni 2024 hadi tarehe 07 Juni 2024 wakiwa na vifaa vilivyoainishwa na JKT kuripoti navyo Makambini.

JKT linawataka Vijana wote walioitwa awamu ya kwanza ambao hawajarioti makambini mpaka sasa, **waripoti mara moja** katika Makambi yaliyo karibu na makazi yao.

Aidha, JKT limetoa nyongeza ya awamu ya pili ya majina ya Vijana waliohitimu elimu ya kidato cha sita mwaka 2024 kujiunga na JKT ili kufanya mafunzo hayo ya Lazima. Vijana hao, waripoti katika Makambi ya JKT yaliyo karibu na mahali wanapoishi.

Vijana hao wote wanatakiwa kuripoti Makambini kuanzia leo hii tarehe 22 Juni 2024 hadi tarehe 26 Juni 2024.

Orodha kamili ya majina ya vijana waliochaguliwa kujiunga na mafunzo hayo awamu ya pili na vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, inapatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.go.tz

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, anawakaribisha Vijana waliohitimu kidato cha sita mwaka 2024 kuungana na Vijana wenzao ili kujengewa Uzalendo, Umoja wa Kitaifa, kufundishwa Stadi za Kazi, Stadi za Maisha na Utayari wa Kulijenga na Kulitumikia Taifa lao.



**Imetolewa na:
Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,
Makao Makuu ya JKT,
Tarehe 22 Juni 2024.**

Vifaa vinavyohitajika Kwa Vijana wa Kujiunga na Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria 2024

1. Bukta ya rangi ya 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni, iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini, isiyo na zipu.
2. T-shirt ya rangi ya kijani (Green Vest).
3. Raba za michezo zenyne rangi ya kijani au blue.
4. Shuka mbili za kulalia zenyne rangi ya blue bahari.
5. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
6. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa zenyne baridi.
7. Track suit ya rangi ya kijani au blue.
8. Nyaraka zote zinazohitajika katika Udhili wa Kujiunga na Elimu ya Juu, zikiwemo cheti vya Kuzaliwa, Vyeti vya Kuhitimu kidato cha Nne nk.
9. Nauli ya kwenda makambini na kurudi nyumbani.